**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO MIFUGO NA UVUVI**

**TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA MKOA WA MWANZA**

# TAARIFA YA USHIRIKA MKOA WA MWANZA KATIKA UZINDUZI WA JUKWAA LA USHIRIKA LA MKOA TAREHE 20 JULAI 2017 KATIKA UKUMBI WA NYANZA CO-OPERATIVE UNION

**IMEWASILISHWA NA:**

SAULO P. LUNYEKA

Kaimu Mrajis wa Vyama Vya Ushirika

Mkoa wa Mwanza

## TAARIFA YA USHIRIKA YA MKOA WA MWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Mkoa wa Mwanza una jumla ya vyama vya Ushirika 735 ambavyo kati ya hivi, vyama vya Ushirika vya mazao ni 228, ushirika wa Akiba na mikopo ni 422,Ushirika wa aina nyingine ni vyama 84 na chama kikuu cha mkoa wa Mwanza – Nyanza cooperative union (1984) Ltd kimoja.

Hata hivyo, kutokana na uhakiki uliofanywa na Tume ya maendeleo ya Ushirika mwezi Juni 2017 katika vyama vyote vya Ushirika mkoa wa Mwanza, uhakiki huu umebaini kuwa kati ya vyama vya Ushirika 735 vilivyopo katika mkoa wa Mwanza, vyama hai ni **102**, sinzia ni **350** na visivyopatikana (not found) ni **283.**

Mgawanyo wa vyama vya Ushirika ki – wilaya ni ifuatavyo:-

| Na | Halmashauri | Vyama hai | Vyama sinzia | Vyama havipo (not found) | Jumla vyama |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Buchosa DC | 4 | 27 | 36 | 67 |
| 2 | Ilemela MC | 11 | 16 | 26 | 53 |
| 3 | Kwimba DC | 11 | 77 | 22 | 110 |
| 4 | Magu DC | 12 | 48 | 23 | 83 |
| 5 | Misungwi DC | 13 | 38 | 97 | 148 |
| 6 | Mwanza CC | 24 | 26 | 29 | 79 |
| 7 | Sengerema DC | 12 | 63 | 47 | 122 |
| 8 | Ukerewe DC | 14 | 55 | 3 | 72 |
| | Chama kikuu | 1 | 0 | 0 | 1 |
| | **JUMLA** | **102** | **350** | **283** | **735** |

## 2.0 MAFANIKIO YA USHIRIKA MKOA WA MWANZA

Katika kipindi cha mwaka 2016/2017 kumekuwepo na mafanikio yafuatayo :-

a) Idadi ya wanachama katika vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo imefikia 51,027(ambapo me 30,206 ke 19,866 na Vikundi/Taasisi 955), vyama vya mazao Wanachama 32,879 ( Ambapo me 23,510 ke 9,369), vyama vingine wanachama ni 2,760 (Ambapo me 1,808 na ke 952).

b) Mtaji katika vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo umefikia 8,056,760,000 (Ambapo hisa 2,176,013,00. Akiba 5,383,876,000 na Amana shs 496,871,000). Vyama vya mazao hisa shs 12,887,000 na vyama vingine hisa shs 92,137,000.

c) Mikopo iliyotolewa katika vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo ni shs 14,631,800,000 kwa shughuli za biashara,kilimo,mifugo na shughuli za kijamii.

d) Ajira katika vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo imefikia waajiriwa 94 katika nafasi mbalimbali za Umeneja, Uhasibu, Afisa mikopo,Ukarani wa mahesabu na ulinzi.

e) Chuo kikuu cha Ushirika Moshi – Tawi la Mwanza kwa ushirikiano na kamati ya Elimu ya Ushirika ya mkoa wa Mwanza , imewezesha mafunzo kwa viongozi na watendaji mbalimbali wa vyama vya ushirika ambapo:

- Wahasibu 53 toka SACCOS 32 wamepata mafunzo ya ufungaji wa vitabu vya mahesabu.
- Wajumbe 65 wa bodi toka SACCOS 30 wamepata mafunzo ya uandaaji wa sera mbalimbali katika SACCOS.
- Wajumbe 48 wa kamati za mikopo toka SACCOS 32 wamepata mafunzo ya usimamizi wa mikopo na tathimini ya mikopo.
- Wajumbe 25 wa kamati ya usimamizi toka SACCOS 14 wamepata mafunzo ya ukaguzi na uchunguzi katika SACCOS.

f) Ukaguzi wa mara kwa mara umefanywa na maafisa Ushirika katika vyama vya ushirika 52 ambapo, Buchosa DC vyama 6 ,Ilemela MC vyama 12, Kwimba DC vyama 3, Magu DC vyama 3, Misungwi DC vyama 5, Mwanza CC vyama 18, Sengerema DC vyama 3 na Ukerewe DC vyama 2.

g) Vyama vya ushirika 44 vimefunga vitabu vyake vya mahesabu na kuwasilisha kwa Shirika la Ukaguzi na Usimamizi la Vyama vya Ushirika (COASCO) Kwa ajili ya ukaguzi wa hesabu zake ambapo:-

- Ukerewe DC vyama 5 vimekaguliwa hesabu za mwaka 2014,2015 na ukaguzi wa 2016 unaendelea.
- Mwanza CC vyama 12 vimekaguliwa hesabu za mwaka 2014,2015 na ukaguzi wa 2016 unaendelea.
- Ilemela MC vyama 11 vimekaguliwa hesabu za mwaka 2014,2015 na ukaguzi 2016 unaendelea.
- Magu DC vyama 6 vimekaguliwa hesabu za mwaka 2014,2015 na ukaguzi 2016 unaendelea.
- Sengerema DC vyama 2 vimekaguliwa hesabu za mwaka 2014,2015 na ukaguzi 2016 unaendelea.
- Misungwi DC vyama 3 vimekaguliwa hesabu za mwaka 2014,2015 na ukaguzi 2016 unaendelea.
- Kwimba DC vyama 4 vimekaguliwa hesabu za mwaka 2013, 2014,2015 na ukaguzi 2016 unaendelea.
- Buchosa DC hakuna vyama vilivyokaguliwa.
- Nyanza Co-operative Union imekaguliwa hesabu za mwaka 2015/2016 na 2016/2017.

h) Katika mwaka 2016/2017, vyama vya ushirika mkoa wa mwanza vimelipa jumla ya shs 19,489,000 katika mfuko wa usimamizi na ukaguzi wa mrajis

wa vyama vya ushirika ambapo, kiwango cha chini ni shs 500,000 kwa SACCOS na shs 300,000 kwa AMCOS na vyama vingine.

i) Katika mwaka 2016/2017, vyama vya Ushirika 86 ndivyo vilivyowasilisha makisio ya mapato na matumizi kwa Mrajis wa vyama vya ushirika ili kuidhinishiwa makisio hayo baada ya kupitishwa na mikutano mikuu ya mwaka ya wanachama ambapo, Buchosa DC vyama 4, Ilemela MC vyama 18, Misungwi DC vyama 10, Magu DC vyama 4, Mwanza CC vyama 18, Kwimba DC vyama 14, Sengerema DC vyama 8 na Ukerewe DC vyama 10.

j) Kwa mwaka 2016/2017, ukomo wa madeni umeidhinishwa katika vyama vya Ushirika vinne(4) vilivyoomba ambapo, Ufumwa SACCOS Tsh 60,000,000/=, Mwandoi SACCOS Tsh 100,000,000/=, Mkukuwami SACCOS Tsh 120,000,000/=, Abajuni SACCOS Tsh 12,000,000/=

k) Kwa mwaka 2016/2017 Mkoa wa Mwanza umesajili vyama vya Ushirika 7 ambapo, Misungwi DC vyama 2, Mwanza CC vyama 2, Sengerema DC chama 1,Buchosa DC chama 1, Kwimba DC chama 1.

## 3.0 FURSA ZA USHIRIKA KATIKA MKOA WA MWANZA

Mkoa wa Mwanza una fursa mbali mbali ambapo zikitumika ipasavyo zinaweza kuleta maendeleo kwa wana ushirika na taifa kwa ujumla,fursa hizi ni pamoja na :-

3.1 Kuwepo kwa Viwanda 11 vya kuchambulia pamba vinavyomilikiwa na nyanza Co- operative union (1984) Ltd , vikifufuliwa vinaweza kuleta ajira na kuchangia katika kukuza uchumi.

3.2 Kuwepo kwa shamba la hekari 650 la Mabuki linalomilikiwa na Nyanza Co-operative union ambalo linaweza kutumika kuzalisha mbegu bora za pamba.

3.3 Kuwepo kwa Taasisi za fedha zinazojihusisha na vyama vya Ushirika kama vile, CRDB BANK, NMB, COVENANT BANK, SELF MF, NSSF N.K.

3.4 Kuwepo kwa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi- Tawi la Mwanza kwa ajili ya Elimu na mafunzo kwa wana Ushirika.

3.5 Kuwepo kwa Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo – SIDO kwa ajili ya maendeleo ya viwanda, mikopo na ujasiriamali.

3.6 Kuwepo kwa maghala ya kuhifadhia mazao (pamba) yapatayo 556 yanayomilikiwa na vyama vya ushirika vya msingi vya mazao 228.

3.7 Kuwepo kwa kiwanda kidogo cha samani Malya kinachomilikiwa na Nyanza co – operative union(1984) Ltd.

3.8 Uwepo wa ziwa Victoria kwa ajili ya shughuli za uvuvi na maeneo ya mabonde kwa ajili ya kilimo cha pamba, mpunga , dengu ,alizeti,kahawa na kilimo cha umwagiliaji.

3.9 Uwepo wa wataalamu mbali mbali na wenye fani mbalimbali katika halmashari za wilaya na ngazi ya mkoa.

## 4.0 CHANGAMOTO YA VYAMA VYA USHIRIKA KATIKA MKOA WA MWANZA

4.1 Kuwepo kwa vyama vya Ushirika 350 sinzia ambapo, sehemu kubwa ya vyama hivi sinzia ni vyama vya ushirika vya msingi vya mazao (AMCOS). Usinzia huu umechangiwa na nyanza kutopata fedha za kununulia mazao kwa wanachama wake tangu msimu 2011/2012.

4.2 Kuwepo migogoro mingi katika vyama vya Ushirika ambayo kwa sehemu kubwa husababishwa na viongozi wa vyama, watendaji wa vyama na wanachama wenyewe wa vyama vya ushirika. Aidha migogoro hii imechochea kuwepo kwa kesi nyingi za Ushirika Mahakamani ambapo mwaka 2016/2017 kuna kesi zipatazo 92 za vyama vya ushirika katika mahakama mbalimbali zilizopo Mkoa wa Mwanza.

4.3 Bodi za watendaji wa vyama vya ushirika kutozingatia sheria,kanuni na masharti ya vyama husika . Hii ni pamoja na vyama vingi kushindwa kufunga

vitabu vyake vya mahesabu, kutokaguliwa na kutofanya mikutano mikuu kwa wakati. Aidha katika mwaka 2016/2017, viongozi wa vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo wa Ukerewe SACCOS,Magu teachers SACCOS, Magu workers SACCOS,Bugogwa SACCOS,Mkukuwami SACCOS na Mwanza poultry multipurpose wamevuliwa nyazifa zao kwa kutozingatia sheria.

4.4 Vyama vingi hususani vya akiba na mikopo kuwa tegemezi kwa mitaji ya nje na hatimaye vyama vingi kudaiwa madeni makubwa na Taasisi za fedha zilizowakopesha.

4.5 Uchache wa Maafisa Ushirika katika Mkoa wa Mwanza ambapo, kwa sasa kuna jumla ya Maafisa Ushirika 25 wanaohudumia vyama vya Ushirika 452 (Hai na Sinzia) vinavyopatikana katika Mkoa wa Mwanza. Aidha mgawanyo wa Maafisa hawa Ki-halmashauri bado haupo sawa kwani kuna kuna Maafisa Ushirika Mkoani 2,Ukerewe DC 1,Magu DC 1,Sengerema DC 1,Misungwi DC 2,Mwanza CC 5,Ilemela MC 3,Kwimba DC 7na Buchosa DC 3.

4.6 Ufinyu wa bajeti na kutokuwepo kwa vitendea kazi muhimu kwa ajili ya kufanya usimamizi wa karibu katika vyama vya ushirika katika wilaya zote za mkoa wa Mwanza.Aidha katika mwaka 2016/2017 Bajeti iliyokuwa imepangwa na Halmashauri kwa sekta ya ushirika na fedha zilizotolewa ni kama ifuatavyo :-

- Misungi DC Shs 4,600,000 Fedha tolewa Shs 3,600,000
- Sengerema DC shs 17,000,000 Fedha tolewa shs 1000,000
- Kwimba DC Shs 8,736,000 Fedha tolewa Hakuna.
- Magu DC Shs 5,000,000 Fedha tolewa Hakuna.
- Buchosa DC Shs 12,000,000 Fedha tolewa Hakuna.
- Ukerewe DC shs 7,262,500 Fedha tolewa hakuna.
- Mwanza CC shs 35,000,000 Fedha tolewa hakuna.
- Ilemela MC shs 25,085,000 Fedha tolewa shs 6,184,000

- Tume ya maendeleo ya ushirika ilitakiwa kutoa pesa katika mkoa wa mwanza Shs 5,846,700 Fedha tolewa shs 2,500,000

4.7 Kuwepo kwa migogoro kati ya viongozi wa vyama vya ushirika vya mazao na baadhi ya serikali za vijiji kuhusu umiliki wa maghala ya vyama vya Ushirika na maeneo yake.

4.8 Maafisa ushirika kutopata mafunzo ya mara kwa mara ili kupata uwezo wa kufanya kazi kwa weledi unaotarajiwa.

4.9 Kutokuwepo uwezeshwaji wa mafunzo kwa wanachama wa vyama vya ushirika kwani sehemu kubwa ya mafunzo ya ushirika inatolewa kwa viongozi na watendaji tu.

4.10 Bodi na watendaji kutowezeshwa kumudu uendeshaji bora wa vyama vyao vya Ushirika.Aidha mafunzo yamekuwa yakitolewa kwa walio karibu na Chuo Kikuu cha Ushirika moshi-Tawi la Mwanza.

4.11 Kuwepo na ubadhilifu/wizi unaofanywa na viongozi ,watendaji na wanachama wa vyama vya Ushirika wasio waaminifu. Ushirikiano umekuwa ukifanywa na viongozi,watendaji na wakopaji wanachama wasio waaminifu kwa kuchukua mikopo mikubwa katika vyama na kuweka dhamana siyo, kisha kukataa / kushindwa kurejesha mikopo hiyo,hatua zinapochukuliwa kwa wadaiwa hao sugu, wamekuwa wakikimbilia Mahakamani au dhamana siyo kutopatikana. Aidha fedha zilizokopeshwa na SACCOS kwa baadhi ya wanachama wake zimeshindwa kurejeshwa tangu 2010 hadi 2017, na hivyo kutishia uhai wa vyama hivyo. Aidha vyama vya ushirika vilivyokubwa na hili ni pamoja na mwanza SACCOS, Victoria SACCOS,Magu Teachers SACCOS,Bugogwa SACCOS, Wadoki SACCOS, Uzinza SACCOS, Vijana ukerewe SACCOS.

4.12 Kumekuwepo na uelewa mdogo wa namna ya ulipaji wa leseni za biashara, kodi ya mapato kwa baadhi ya vyama vya ushirika.

## 5.0 MIKAKATI YA KUIMARISHA VYAMA VYA USHIRIKA KATIKA MKOA WA MWANZA

a. Kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa mara kwa mara katika vyama vya ushirika ili kujenga nidhamu ya udhibiti wa fedha na mali zingine za vyama za vyama pamoja na kuzuia ubadhilifu usitoke na kuzuia migogoro mipya.
b. Kufufua vyama vya ushirika sinzia kwa kuimarisha nyanza co-operative union na vyama vya ushirika vya msingi vya mazao kwa wanachama wa vyama vya mazao waelimishwe umuhimu wa kukusanya mazao yao katika vyama vyao vya Ushirika kama vile pamba, mpunga, dengu,kahawa na alizeti.
c. Vyama vya Ushirika viweke mikakati ya kuimarisha mitaji ya ndani kila Mwaka.
d. Vyama vya Ushirika vipime maeneo yake na viwe na hati miliki ya mali yake.
e. Vyama vya Ushirika viangalie fursa ya kuanzisha na kuwekeza katika Viwanda katika mkoa wa Mwanza kwa kutumia fursa zilizopo.
f. Vyama vya Ushirika viwe vinatenga asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya Elimu na mafunzo ya wanachama wake, viongozi na watendaji wa vyama kila mwaka.
g. Kuhakikisha vyama vya ushirika vinatumia bajeti iliyoidhinishwa na Mrajis wa vyama vya Ushirika, vinafunga vitabu na kukaguliwa kwa wakati.
h. Elimu iendelee kutolewa kwa viongozi , watendaji , wanachama na wadau wa ushirika kuwa migogoro kati yao inapaswa kupelekwa kwa mrajis wa vyama vya ushirika.

## HITIMISHO

Vyama vya Ushirika vitaendelea kushamiri na kuimarika iwapo kutakuwepo na Utamaduni wa kukuza Mitaji ya ndani katika vyama hivyo, uendeshaji bora wa vyama hivyo kwa kuzingatia Sheria ya ushirika Na. 6 ya mwaka 2013, Kanuni zake pamoja na masharti ya Vyama husika.